**MTIHANI WA MWIGO WA GATUZI NDOGO LA GATANGA 2016**
**102/3**
**KARATASI YA TATU**
**FASIHI**

**SEHEMA YA A: USHAIRI**

1. **Lazima.**
**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**(alama 20)

**Barabara.**
Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimechoka tiki
Natamani kuketi
Ninyooshe misuli
Nitulize akili

Lakini

Azma yanisukuma
Mbele ikinihimiza kuendelea
Baada ya miinuko na kuruba
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi.

Punde natumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ili pupanda tena
Ghafla nakumbuka ilivyosema
Ile sauti zamani kidogo
"Kuwa tayari kupanda na kushuka."

Ingawa nimechoka
Jambo moja li dhahiri
Lazima niifuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka
Nipande na kushuka.

Jambo moja nakumbuka: Mungu
Je, nimwombe tena? Hadi lini?
Labda amechoshwa na ombaomba zangu
Nashangaa tena!

Kitu kimoja nakiamini
Lazima niendelee kujitahidi kwa kila hatua mpya
Nijikokote kuiandama hii barabara yenye ukungu
Nikinaswa na kujinasua
Yumkini nitafika mwisho wake
Ikiwa wangu mwisho haitauwahi kabla.

*(Timothy Arege)*

**Maswali.**

(a) Taja na ueleze aina ya shairi hili. (alama 2)
(b) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
(c) Fafanua dhamira ya shairi hili. (alama 2)
(d) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. (alama 3)
  (i) Tanakali za sauti.
  (ii) Mbinu rejeshi
  (iii) Taswira
(e) Eleza umhimu wa maswali balagha katika shairi. (alama 2)
(f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 4)
(g) Eleza matumizi ya mistari mishata katika shairi hili. (alama 2)
(h) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi. (alama 3)
  (i) Kuruba
  (ii) Siha
  (iii) Machweo

for more past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU B: RIWAYA.**
**Ken Walibora: Kidagaa Kimwemwozea.**
**Jibu swali la 2 au la 3**

2. "Nilikuwa nimekwenda ibada kaka."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Ni ibada gani anayozungumizia msemaji. (alama 1)
   (c) Hii ibada imemfanya akose kuwajibika. Thibitisha. (alama 6)
   (d) Eleza **sifa** zozote tano za msemewa. (alama 5)
   (e) Eleza umuhimu wa msemaji wa kauli hii. (alama 4)

3. Jadili jinsi mwandishi wa Kidagaa Kimemwozea anashughulikia maudhui yafuatayo;
   (a) Kisasi (alama 10)
   (b) Usaliti (alaam 10)

**SEHEMU C: TAMTHILIA**
**Timothy Arege: Mstahiki Meya**
**Jibu swali la 4 au la 5**

4. Haki yetu!
   Jasho letu!
   Haki yetu!
   Jasho letu!
   Damu yetu!
   (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Eleza kwa tafsili haki, jasho na damu inayorejelewa. (alama 10)
   (c) Fafanua sifa zozote **sita** za anayeelekezewa kilio hiki. (alama 6)
5. Onyesha matumizi ya mbinu zifuatazo katika tamthilia;
   (i) Uzungumzi nafsiya. (alama 5)
   (ii) Majazi (alama 8)
   (iii) Taswira (alama 7)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**
**Ken Walibora na S.A Mohamed (wah): Damu Nyeusi na Hadithi nyingine.**
**Damu Nyeusi (K. Walibora)**

6. "Msifikiri kwamba mzungu anatupenda sisi watu weusi." ;
   (a) Eleza ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi ya Damu Nyeusi. (alama 10)
   (Tazama na Mauti - S.A. Mohamed)
   (b) "... Lakini yeye hataki riziki, anataka muluki."
      (i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
      (ii) Fafanua sifa **sita** za mrejelewa. (alama 6)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI.**

7. (a) (i) Eleza tofauti ya ngoma na ngomezi. (alama 2)
      (ii) Taja aina **nne** za ngomezi za kisasa. (alama 4)
   (b) (i) Mivigha ni nini? (alama 2)
      (ii) Eleza sifa zozote **nne** za miviga. (alama 4)
   (c) Fafanua majukumu ya michezo ya watoto (chekechea) (alama 8)

for more past papers visit: www.freekcsepastpapers.com